

Nini tafsiri ya jina Adamu,

Adamu ni neno la kiebrania lenye maana ya “wa udongo” yaani aliyetokana na *udongo/ardhi*. Mtu wa kwanza kuumbwa alipewa jina hilo Adamu na Mungu mwenyewe kufuatia asili yake alipotolewa.

Mwanzo 2:7 “Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai”.

Na jina “Adamu” hakupewa mtu mmoja tu bali wote wawili (*yaani mwanamume na mwanamke*)

Mwanzo 5:1” Hiki ndicho kitabu cha vizazi vya Adamu. Siku ile Mungu alipoumba mtu, kwa sura ya Mungu alimfanya;

2 mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki AKAWAITA JINA LAO ADAMU, siku ile walipoumbwa”.

Kwa urefu na kina Zaidi, kwanini Mungu awape wote wawili jina moja fungua hapa >>> Kwanini Mungu aliwaita Adamu na Hawa jina moja?

Watoto wote waliozaliwa baada ya Adamu, wakitwa Wana-damu. (*wana wa aliyekuwa wa udongo*). Hivyo na sisi wote asili ya miili yetu ni ardhini, ndio maana tunakufa na miili yetu inaoza ardhini.

Lakini baada ya maisha haya, kama tukishinda vita vya kiimani vya ulimwenguni, maandiko yanasema tutavikwa miili mipya ya kimbinguni, hivyo hatutaitwa tena wanadamu, wala hatutaishi kwa kula na kunywa kama wanyama, wala tamaa za mwili hazitakuwepo tena bali tutakuwa kama Malaika kwasababu tutapewa miili mingine isiyo ya udongo.

Marko 12:25 "Kwa maana watakapofufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika walioko mbinguni".

Je una tumaini la kuvikwa mwili mpya wa kimbinguni?..

Kumbuka tumaini hilo na uhakika huo tunaupata tu endapo tupo ndani ya Kristo, na tunaishi maisha yanayompendeza yeye.

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

Mungu anatufundisha kusamehe mara saba sabini, ila Kwanini yeye hakumsamehe Adamu alipoasi?.

Tofauti kati ya mtu na mwanadamu ni ipi?

KWANINI YESU NI ADAMU WA PILI?

Kwanini Kristo aitwe Mwana-kondoo. (Yohana 1:29)

JE! Kaini alimpatia mke wake wapi?

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp